

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630

Nukushi: +255 (026) 2963629

Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz

Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

WANAFUNZI WILAYANI MASWA WANUFAIKA NA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI

Wanafunzi wenyе umri wa miaka 6 hadi 18 kutoka kwenye kaya maskini wilayani Maswa mkoani Simiyu wamenufaika na ruzuku inayotolewa na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwa kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kununulia vifaa vya shule vinavyowawezesha kupata elimu bora.

Hayo yamesemwa na Katibu Tawala Mkoa wa Simiyu Bw. Jumanne A. Sagini kuitia taarifa yake aliyoiwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa wakati wa ziara ya kamati hiyo yenyе lengo la kukagua miradi ya maendeleo inayoteklezwa na Ofisi ya Rais – Utumishi na TAMISEMI.

Bw. Sagini amesema, uwepo wa TASAF umechangia ongezeko kubwa la uandikishwaji watoto shulenii, hivyo watoto wenyе umri wa miaka 6 hadi 18 kutoka kwenye kaya maskini wameweza kuandikishwa shule na mahudhurio yao ni zaidi ya asilimia 80. Pia, ameeleza kuwa TASAF imepunguza wimbi la ajira za watoto waliopo katika kaya maskini.

Aidha, Bw. Sagini ameongeza kuwa kaya kaya **6,120** sawa na asilimia **52** ya walengwa wa TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi wamewezeshwa kulima pamba ekari 8,712 katika msimu wa 2017/2018.

Akizungumza na wananchi na wanafunzi wa shule ya Nyalikungu Sekondari, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Mhe. Jason Rweikiza (Mb) amewataka wanafunzi

kuzingatia masomo ili ruzuku inayotolewa na TASAF iwe na manufaa kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Pia Mhe. Rweikiza ametoa wito kwa wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini mkoani Simiyu kuhakikisha wanatumia vizuri pesa wanayoipata kuitia TASAF na kuwataka kuiga mfano mzuri wa Bi. Monica Kwilasa ambaye ametumia vema pesa anayopatiwa na TASAF kwa kujenga nyumba nzuri.

Kwa upande wake, mnufaika huyo wa kaya maskini Bi. Monica Kwilasa ameishukuru Serikali kwa kuwapelekea Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ambao umemuwezesha kuwanunulia wajukuu zake sare za shule,kuendesha biashara ya mama lishe na hatimaye kujenga nyumba yake.

Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora, Kapteni (Mstaafu) Mhe. George H. Mkuchika (Mb) amewaeleza wananchi na wanafunzi wa Nyalikungu Sekondari, kuwa lengo la ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge na Utawala na Serikali za Mitaa ni kujiridhisha na matumizi ya pesa za Serikali zinazotolewa na TASAF.

Akiwahasa wanufaika wa TASAF, Kapteni (Mstaafu) Mhe. George H. Mkuchika (Mb) amewataka wananchi na wanafunzi wa Nyalikungu Sekondari kuhakikisha fedha za uhawilishaji wanazozipokea toka TASAF zinatumika kwa manufaa na zinawasaidia kuwaondoa katika hali ya umaskini.

Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unatekelezwa katika Wilaya zote Tano za Mkoa wa Simiyu ambazo ni Bariadi, Maswa, Busega, Meatu na Itilima. Aidha, katika Mkoa wa Simiyu jumla ya Vijiji **329** vyenye Kaya **41,575** zilizosajiliwa katika Mpango.

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
OFISI YA RAIS (UTUMISHI)
TAREHE 17 MACHI, 2018**